

*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:.....*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

**01**

**KISWAHILI**

**Muda: 1: 30**

**Jumatano, 25 Oktoba, 2023 Asubuhi.**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina jumla ya maswali **matano (05)**.
2. Jibu Maswali yote.
3. Andika Namba yako ya Upimaji katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.

<b>KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU</b>		
<b>NAMBA YA SWALI</b>	<b>ALAMA</b>	<b>SAHIHI YA MPIMAJI</b>
1		
2		
3		
4		
5		
<b>JUMLA</b>		
<b>SAHIHI YA MHAKIKI</b>		

**Ukurasa wa 1 kati ya 5**

Find this and other free resources at:

<https://maktaba.tetea.org>

*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:.....*

**SEHEMU A: IMLA (ALAMA 10)**

1. Sikiliza kwa makini sentensi zifuatazo kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

- i) \_\_\_\_\_
- ii) \_\_\_\_\_
- iii) \_\_\_\_\_
- iv) \_\_\_\_\_
- v) \_\_\_\_\_

**SEHEMU B: NYAKATI MBALIMBALI (ALAMA 10)**

2. Sentensi zifuatazo zipo katika wakati gani? **Andika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi. Sentensi (i) imetumika kama mfano.

- i) Kaka anaimba nyimbo vizuri.

**Wakati uliopo.**

- ii) Daktari alimtibu mgonjwa wetu

---

- iii) Baba yangu ataandika barua

---

- iv) Wanafunzi wanafanya mtihani wao.

---

- v) Kuku walitaga mayai mengi.

---

- vi) Baba na mama watalima shamba lote.

---

**Ukurasa wa 2 kati ya 5**

*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:.....*

### **SEHEMU C: KUTEGUA VITENDAWILI (ALAMA 10)**

3. Kamilisha vitendawili vifuatavyo kwa kuchagua maneno yaliyopo kwenye mabano na kuyaandika katika nafasi zilizoachwa wazi.
- Askari wangu mpole lakini adui wanamhara \_\_\_\_\_(paka, mbwa, mbuzi)
  - Bibi hachoki kunibeba \_\_\_\_\_(kiti, kochi, kitanda)
  - Nyumba yangu ina nguzo moja \_\_\_\_\_ (kalamu, uyoga, mlango)
  - Mzungu katoka ulaya na mkono kiunoni \_\_\_\_\_ (mkoba, ndoo, kikombe)
  - Tajiri wa rangi \_\_\_\_\_ (nyumba, mawingu, kinyonga)

### **SEHEMU D: UTUNGAJI (ALAMA 10)**

4. Sentensi zifuatazo zimechanganywa. Zipange katika mtiririko unaoleta maana kwa kuandika herufi A, B, C, D, na E katika nafasi ulizopewa.

Sentensi ya (i) imetumika kama mfano.

- Hatimaye Kaposo alipelekwa hospitali. **F**
- Nyuki walikasirika, wakamfukuza na kumuumma Kaposo.\_\_\_\_\_
- Siku moja Kaposo alitoroka shule na kwenda msituni.\_\_\_\_\_
- Alirusha jiwe likapiga kwenye mzinga wa nyuki.\_\_\_\_\_
- Alikuwa akitumia manati yake kuwinda ndege.\_\_\_\_\_
- Huko msituni Kaposo alikwenda kuwinda ndege.\_\_\_\_\_

**Ukurasa wa 3 kati ya 5**

*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:.....*

### **SEHEMU E: UFAHAMU (ALAMA 10)**

5. Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

*Uhai wa binadamu, wategemea mimea,  
Mazingira ni muhimu, hakika twategemea,  
Miti yetu ni adhimu, mvua twajipatia,  
Pokea zangu salamu, tuhifadhi mazingira.*

*Kukulinda ni muhimu, miti yetu asilia,  
Juhudi kila awamu, kuitunza asilia,  
Miti ni zao muhimu, **samani** twajipatia,  
Pokea zangu salamu, tuhifadhi mazingira.*

*Tumeishika hatamu, azima kuifikia,  
Shughuli za binadamu, hakika zinachangia,  
Kuuharibu utamu, wa miti na hewa pia,  
Pokea zangu salamu, tuhifadhi mazingira.*

#### **Maswali:**

- a) Mwandishi wa shairi anasisitiza tulitunze zao gani?

- 
- b) Taja faida mbili tunazozipata kutokana na kutunza miti.

i) \_\_\_\_\_

ii) \_\_\_\_\_

- c) Nini kinasababisha uharibifu wa mazingira?

- 
- d) Nini maana ya neno “samani”?

---

**Ukurasa wa 4 kati ya 5**

*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi:.....*

e) Katika ubeti wa pili mwandishi anatoa ujumbe gani?

---

**Ukurasa wa 5 kati ya 5**